JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU MHESHIMIWA DKT. MARY MICHAEL NAGU (MB) AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA UCHUMI 2014 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2015/16

OFISI YA RAIS, TUME YA MIPANGO
JUNI, 2015

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU MHESHIMIWA DKT. MARY MICHAEL NAGU (MB) AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA UCHUMI 2014 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2015/16

UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi 2014 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16. Pamoja na hotuba hii nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2014 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2015/16. Taarifa ya hali ya uchumi na Mpango ninayowasilisha ndio msingi wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/16.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kushiriki Mkutano wa 20 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni mkutano wa Bunge la Bajeti na wa mwisho kwa Serikali ya Awamu ya nne. Aidha, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha majadiliano ya Mpango wa Maendeleo kwa umakini na umahiri mkubwa tangu yalipoanza mwaka 2011/12 hadi sasa. Nashukuru pia kwa fursa ya hii leo kuwasilisha hotuba yangu.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia nafasi hii kipekee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tume ya Mipango, na wasaidizi wake wakuu, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal Makamu wa Rais, na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb) Waziri Mkuu, kwa uongozi wao mahiri kwa kipindi chote cha awamu ya nne. Chini ya uongozi wao, uchumi wa Taifa umeimarika na Taifa limepiga hatua kubwa kimaendeleo kutokana na usimamizi thabiti wa utekelezaji wa Mipango, Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Programu, na Mikakati mbalimbali ya maendeleo.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, Mbunge wa Magu, kwa maoni na ushauri iliyotupatia.

Tulizingatia ushauri wa Kamati na tunaahidi kuzingatia ushauri huo katika hatua mbalimbali za uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Grace Khwaya Pujah (Mb) na Mheshimiwa Dkt Innocent Rwabushaija Sebba (Mb) kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kutumia fursa hii kutoa salamu za pole kwako na kwa Wabunge wote, kwa kuondokewa na wabunge wenzetu, Mhe. Salmin Awadh Salmin aliyekuwa mwakilishi wa jimbo la Magomeni – Zanzibar, Mhe. Capt. John Damiano Komba aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi, na Mhe. Eugen Elishiringa Mwaiposa, aliyekuwa Mbunge wa Ukonga. Vilevile, natoa pole kwa familia za marehemu, ndugu na wananchi wa majimbo hayo. Pia, nawapa pole wabunge wote waliopoteza wapendwa wao. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Aidha, natoa salamu za pole kwa wananchi wote waliopatwa na maafa mbalimbali katika mwaka huu wa fedha.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine ninawiwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Hanang kwa kuendelea kuniunga mkono na kunipa ushirikiano katika kazi za Jimbo pamoja na majukumu yangu mengine ya Kitaifa. Wananipenda nami nawapenda. Wameomba nigombee tena, nami nawajulisha kuwa nimepokea ombi lao na nitagombea ili niendelee kuwatumikia kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Safari ya kuwatumikia ilianza mwaka 2005 mpaka 2010 mliponipa ridhaa ya kuwatumikia tena na ni matumaini yangu kwamba mtanipa fursa tena mwaka huu ili tuendelee kuimarisha maendeleo ya Wilaya yetu. Kipekee napenda kuishukuru sana familia yangu inayoongozwa na Prof. Joseph Tarmo Nagu kwa upendo, uvumilivu na kuendelea kunitia moyo katika kazi zangu za kila siku. Naamini bila ushirikiano wenu kazi ingekuwa ngumu sana.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba ninayowasilisha imegawanyika katika sehemu kuu nne: kwanza ni maelezo mafupi kuhusu mwenendo wa hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2014; pili ni muhtasari wa mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa

Taifa 2014/15; tatu ni miradi ya Kitaifa ya kimkakati ambayo Serikali inatarajia kutekeleza katika mwaka 2015/16; na nne ni ugharamiaji wa Mpango, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba sasa nieleze kwa muhtasari mwenendo wa hali ya uchumi kwa mwaka 2014.

MWENENDO WA HALI YA UCHUMI 2014

Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

10. ***Mheshimiwa Spika,*** taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa ya Aprili 2015, inaonesha kuwa Pato la Dunia lilikua kwa wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2014, sawa na ukuaji ulivyokuwa mwaka 2013. Hali hiyo ilichangiwa na: kuongezeka kwa ukuaji wa uchumi katika nchi zilizoendelea kutoka asilimia 1.4 mwaka 2013 hadi asilimia 1.8 mwaka 2014; kushuka kwa ukuaji wa uchumi wa nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea kutoka asilimia 5.0 mwaka 2013 mpaka asilimia 4.6 mwaka 2014; kushuka kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara kutoka asilimia 5.2 mwaka 2013 mpaka asilimia 5.0 mwaka 2014; migogoro ya kisiasa katika nchi mbalimbali; kushuka kwa bei za nishati ya mafuta katika soko la dunia; na sera za kubana matumizi kwa nchi mbalimbali hususan za ukanda wa Ulaya.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** Pato la Dunia linatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2015 na asilimia 3.8 mwaka 2016. Aidha, kwa nchi zilizoendelea, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuwa asilimia 2.4 mwaka 2015 na 2016. Ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea unatarajiwa kuwa asilimia 4.3 mwaka 2015 na asilimia 4.7 mwaka 2016. Kwa upande wa nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuwa asilimia 4.5 mwaka 2015 na kuongezeka hadi asilimia 5.1 mwaka 2016. Hivyo, kwa ujumla, matarajio ya mwenendo wa uchumi wa Dunia kwa mwaka 2015 na mwaka 2016 ni kuendelea kuimarika kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea, na kupungua kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoibukia kiuchumi hususan nchi zinazotegemea mauzo ya mafuta kwa kiwango kikubwa kufuatia kushuka kwa bei ya nishati hiyo katika soko la dunia.

Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

- **Pato la Taifa**

12. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014, Pato la Taifa (Tanzania Bara) lilikua kwa wastani wa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 7.3 mwaka 2013. Pato la Taifa 2014 (kwa bei za mwaka husika) lilikuwa shilingi trilioni 79.4 sawa na wastani wa pato la kila mtu la shilingi 1,724,416 (Dola za Kimarekani 1,038) ikilinganishwa na shilingi trilioni 70.9 mwaka 2013 sawa na wastani wa pato la kila mtu la shilingi 1,582,797 (Dola za Kimarekani 948). Hivyo, jitihada kubwa zaidi zinahitajika kufikia lengo lililowekwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo la dola za Kimarekani 3,000 ifikapo 2025.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014, shughuli za kiuchumi zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji ni: ujenzi asilimia 14.1 ikilinganishwa na asilimia 14.6 mwaka 2013; usafirishaji na uhifadhi mizigo asilimia 12.5 ikilinganishwa na asilimia 12.2 mwaka 2013; fedha na bima asilimia 10.8 ikilinganishwa na asilimia 6.2 mwaka 2013; na biashara na matengenezo asilimia 10.0 ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2013. Aidha, ukuaji wa shughuli za kiuchumi za kilimo ambayo inajumuisha mazao, ufugaji, misitu na uvuvi ulikuwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2013.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla, katika kipindi cha kuanzia 2006 hadi 2014, Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 6.4. Kiwango hiki ni chini ya lengo la asilimia 8 kwa mwaka lililowekwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Hata hivyo, ukuaji huu umewezesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 20 duniani ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa na kuzidi wastani wa ukuaji wa uchumi wa asilimia 5.2 kwa nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini ya mchango wa shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa mwaka 2014 katika Pato la Taifa inaonesha kuwa sekta ya huduma ndiyo inayochangia sehemu kubwa ya Pato la Taifa (asilimia 41.3). Hata hivyo, sekta ya kilimo bado inatoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa (asilimia 28.9). Mchango wa sekta ya viwanda na ujenzi ni asilimia 21.7 ambapo uzalishaji wa bidhaa za viwandani unachangia asilimia 5.6.

- **Mfumuko wa Bei**

16. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014 na robo ya kwanza ya mwaka 2015, mfumuko wa bei nchini uliendelea kubaki katika kiwango cha tarakimu moja. Aidha, mwaka 2014 wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 6.1 ikilinganishwa na asilimia 7.9 mwaka 2013. Hata hivyo, mwenendo wa mfumuko wa bei katika mwaka 2014 ulikuwa ukibadilika badilika ambapo Januari 2014 ulikuwa asilimia 6.0 na kuongezeka hadi asilimia 6.7 Agosti 2014 na kushuka hadi asilimia 4.8 Desemba 2014. Katika kipindi husika, mfumuko wa bei za vyakula ulishuka kutoka asilimia 6.6 Januari 2014 hadi asilimia 5.7 Desemba 2014. Mfumuko wa bei za bidhaa za nishati ulishuka kwa kiwango kikubwa kutoka asilimia 18.7 Januari 2014 hadi asilimia 6.2 Desemba 2014. Hadi Machi 2015, wastani wa mfumuko wa bei uliendelea kushuka na kufikia asilimia 4.3 na kupanda kidogo hadi 4.5 Aprili 2015.

- **Thamani ya Shilingi**

17. ***Mheshimiwa Spika,*** wastani wa kiwango cha kubadilisha dola ya Kimarekani dhidi ya shilingi ya Tanzania ilikuwa shilingi 1,653.1 mwaka 2014 ikilinganishwa na shilingi 1,598.6 mwaka 2013. Hadi Machi 2015, dola moja ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 1,786.3. Kushuka kwa thamani ya shilingi kulitokana na: kuongezeka kwa thamani ya dola ya Marekani kulikosababishwa na kuimarika kwa uchumi wa nchi hiyo; kuongezeka kwa mahitaji makubwa ya Dola ya Kimarekani kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka nje hususan kuwezesha uwekezaji mkubwa katika sekta mbalimbali za kiuchumi nchini; iliyotokana na ukweli kuwa ukubwa na thamani ya bidhaa na huduma zinazouzwa nje ya nchi kuwa bado ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji ya fedha za kigeni kuwezesha uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje.

- **Mauzo ya Bidhaa Nje**

18. ***Mheshimiwa Spika,*** thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi ilifikia Dola za Kimarekani milioni 8,769.3 mwaka 2014 ikilinganishwa na dola milioni 8,459.7 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 2.8. Aidha, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi ilifikia Dola za Kimarekani milioni 13,623.2 mwaka 2014 kutoka dola milioni 13,517.6 mwaka 2013. Hivyo, urari wa biashara katika mwaka 2014 ulikuwa na nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 4,853.9.

- **Akiba ya Fedha za Kigeni**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** akiba ya fedha za kigeni ilipungua kutoka Dola za Kimarekani million 4,676.2 kwa kipindi kinachoishia Desemba 2013 hadi Dola za Kimarekani milioni 4,383.6 Desemba 2014. Hadi Machi 2015, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola milioni 4,064.8 sawa na uwezo wa kuagiza bidhaa nje kwa kipindi cha miezi minne. Hali hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka mahitaji ya uagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi.

- **Mapato na Matumizi**

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2014 hadi Aprili 2015, jumla ya mapato ya Serikali yakijumuisha ya Halmashauri yalikuwa shilingi trilioni 8.641 sawa na asilimia 86 ya makadirio ya shilingi trilioni 9.991. Lengo hilo halikufikiwa kutokana na makusanyo madogo ya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi yaliyotokana na mwitikio mdogo wa matumizi ya mashine za kielektroniki za ukasanyaji wa kodi, kuchelewa kuwasilishwa kwa makusanyo ya mapato katika Halmashauri, na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje. Aidha, matumizi ya Serikali katika kipindi husika yalikuwa shilingi trilioni 14.121 ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi trilioni 11.543 na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi trilioni 2.578.

- **Deni la Taifa**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi 2015, deni la Taifa lilifikia Dola za Kimarekani bilioni 19.48 sawa na shilingi trilioni 35.01 ikilinganishwa na dola bilioni 18.67 sawa na shilingi trilioni 30.6 Machi 2014. Sababu kubwa ya ongezeko hili ni riba na madeni mapya yaliyokopwa na Serikali kwa ajili ya kugharamia ujenzi na ukarabati wa miundombinu hususan ya usafirishaji na nishati.

- **Mwenendo wa Viashiria vya Umaskini**

22. ***Mheshimiwa Spika****,* kwa mujibu wa Tafiti za Mapato na Matumizi ya Kaya, umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kutoka asilimia 39 mwaka 1991/92, asilimia 35.6 mwaka 2000/01 hadi asilimia 33.6 mwaka 2007 na kuendelea kushuka hadi asilimia 28.2 mwaka 2011/12. Kwa ujumla umaskini wa chakula, umepungua kutoka asilimia 21.6 mwaka 1991/92, asilimia 18.7 mwaka 2000/01 hadi asilimia 11.3 mwaka 2007 na kuendelea kupungua hadi asilimia 9.7 mwaka 2011/12.

23. ***Mheshimiwa Spika****,* kwa upande wa vijijini, umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kutoka asilimia 40.8 mwaka 1991/92, hadi asilimia 39.4 mwaka 2007 na kuendelea kushuka hadi asilimia 33.3 mwaka 2011/12. Umaskini wa mahitaji ya msingi kwa maeneo ya mijini (isipokuwa Dar es Salaam) umepungua kutoka asilimia 28.7 mwaka 1991/92, hadi asilimia 22.7 mwaka 2007 na kuendelea kushuka hadi asilimia 21.7 mwaka 2011/12. Kwa upande wa jiji la Dar es Salaam, umaskini umepungua kutoka asilimia 14.1 mwaka 2007 hadi asilimia 4 mwaka 2011/12.

24. ***Mheshimiwa Spika****,* takwimu hizi zinaonesha kuwa kiwango cha umasikini vijijini kimepungua kwa asilimia 6.1 katika kipindi cha miaka mitano ya karibuni (2007 - 2011/12) ikilinganishwa na asilimia 1.4 tu katika kipindi cha miaka 15 kati ya mwaka 1991/92 mpaka 2007. Mwenendo huu unaashiria kuwa ukuaji wa uchumi kuendelea kukua kwa kasi kubwa (wastani wa asilimia 6.4 kwa mwaka) kwa kipindi cha takriban miongo miwili sasa, umeanza kuzaa matunda kwa maana ya kupunguza umaskini kwa kasi kubwa na kuwanufaisha wananchi wengi zaidi.

25. ***Mheshimiwa Spika***, maelezo ya kina kuhusu hali ya uchumi yapo katika Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2014 na Kitabu cha Mpango wa Maendeleo, sura ya kwanza **(Uk 1 hadi 8).**

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2014/15

26. ***Mheshimiwa Spika,*** sasa naomba nieleze kwa ufupi kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/15, kwa kipindi kinachoishia Mei 2015.

Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati

27. ***Mheshimiwa Spika****,* katika eneo la **reli,** kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: ununuzi wa vichwa vipya 13 vya treni ambapo vichwa 7 tayari vimepokelewa; kupokelewa kwa mabehewa mapya 22 ya abiria na kuanza kutumika katika huduma ya treni maalum (Deluxe), mabehewa 197 mapya ya mizigo, mabehewa 17 ya breki na mabehewa 25 ya kubebea kokoto.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **barabara** hatua iliyofikiwa ni pamoja na:- kukamilika kwa ujenzi wa kilometa 504.6 za barabara kuu kwa kiwango cha lami ikilinganishwa na lengo la kilometa 539, na ukarabati wa kilometa 87.8 za barabara kuu kwa kiwango cha lami ikilinganishwa na lengo la kilometa 165. Baadhi ya barabara zilizokamilika ni: Tunduma – Sumbawanga (km 223.2); Isaka – Ushirombo (km 132); Korogwe – Handeni – Mkata (km 120.3); Ndundu – Somanga (km 60); na Migori – Dodoma (km 164.7) katika barabara ya Iringa – Dodoma. Aidha, ukarabati wa barabara ya Itoni - Mkiu – Liganga na Mchuchuma kwa kiwango cha changarawe umekamilika.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **madaraja** hatua iliyofikiwa ni: ujenzi wa daraja la Mbutu (Tabora) asilimia 99, Kigamboni (Dar es Salaam) asilimia 88, Kavuu (Rukwa) asilimia 40, Kilombero (Morogoro) asilimia 26, Lukuledi II (Mtwara) asilimia 25 na Sibiti (Singida) asilimia 22.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **bandari**, hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kukamilika kwa taarifa ya uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya huduma ya kusimamia na kuimarisha gati Na. 1 – 7 na ujenzi wa gati la magari katika bandari ya Dar es Salaam; kukamilika kwa tathmini ya mali katika eneo la bandari ya Mbegani - Bagamoyo; na kufunguliwa kwa zabuni kwa ajili ya ujenzi wa magati 4 katika bandari ya Mtwara.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **sekta ya nishati,** hatua iliyofikiwa ni pamoja na: ujenzi wa kituo cha kufua umeme Kinyerezi I kukamilika kwa asilimia 88 ambapo kazi zinazoendelea ni pamoja na: ujenzi wa vituo vya kupoza na njia za kusafirisha umeme; ujenzi wa karakana, majengo ya utawala na barabara za ndani katika eneo la mradi. Aidha, ukamilishaji wa ulipaji fidia unaendelea katika mradi wa usafirishaji umeme wa Makambako – Songea na ujenzi wa nguzo za njia ya umeme katika mradi wa msongo wa kV 400 wa Iringa – Shinyanga unaendelea.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **miradi ya maji** kazi zilizofanyika ni: kukamilika kwa ujenzi wa miradi mipya 684, na upanuzi na ukarabati wa miradi 241 ya maji vijijini; na ulazaji wa mabomba katika mradi wa maji Ruvu Chini kutoka Bagamoyo hadi Dar es Salaam umekamilika kwa km 54.43 kati ya km 55.93 za mradi sawa na asilimia 97. Aidha, katika mradi wa maji Ruvu Juu, kazi ya upanuzi

wa chanzo cha maji eneo la Ruvu darajani na mitambo ya kusafisha maji eneo la Mlandizi inaendelea ambapo ujenzi umefikia asilimia 64.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **sekta ya kilimo,** kazi zilizotekelezwa ni upimaji wa mashamba makubwa 9 ya uwekezaji ya Mpanga - Ngalamila, Lukulilo, Bagamoyo, Kasulu, Muhoro, Tawi, Kitengule, Mkulazi na Pangani. Aidha, kati ya mashamba hayo, mashamba 4 ya Bagamoyo, Lukulilo, Kitengule na Mkulazi yamepata hatimiliki na mashamba 3 yamepata wawekezaji isipokuwa shamba la Mkulazi.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** kwenye **Skimu za umwagiliaji wa mpunga**, hatua iliyofikiwa ni pamoja na: ujenzi wa skimu 19 zenye jumla ya hekta 9,531 ambao utawanufaisha wananchi 69,681 umefikia asilimia 40; kampuni za RUDI na UNIQUE zimepewa kazi ya kuendesha skimu 30 za umwagiliaji; na kukamilika kwa ujenzi wa maghala 2 chini ya Mfumo wa Hifadhi na Uuzaji wa Pamoja katika Wilaya ya Mlele (Katavi).

35. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **maendeleo ya mifugo**, Serikali imeendelea kuimarisha minada ya upili kwa kukarabati minada ya Pugu (Ilala), Lumecha (Songea), Kirumi (Butiama) na Nyamatala (Misungwi). Vile vile, ujenzi wa barabara kuzunguka mnada wa Kizota (Dodoma) umekamilika pamoja na ukarabati wa nyumba za watumishi na kusimika mzani. Aidha, wilaya za Busega, Igunga na Kiteto zimeainisha na kutenga maeneo ya ufugaji yatakayotumika kuanzisha shamba darasa la kufundishia wafugaji kuhusu uzalishaji, uvunaji na uhifadhi wa malisho yenye jumla ya ekari 42.5. Kwa upande mwingine, Serikali imeagiza vifaa vya uhamilishaji ikiwemo mitungi 9 na ununuzi wa mbegu za malisho.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **uvuvi**, mwongozo wa utoaji wa ruzuku kwa wavuvi na wafugaji wa samaki umeandaliwa na utawawezesha kupata ruzuku kwa kuchangia asilimia 60 ya gharama ya zana na pembejeo. Aidha, Serikali iliendelea kuimarisha kituo cha Machui (Tanga) kwa kujenga mabwawa 2 ya kufugia samaki na kukamilisha ujenzi wa jengo la kutotolea vifaranga vya samaki; kuanzishwa kwa vituo 2 vya ukuzaji wa samaki wa maji baridi vya Mwamapuli – Igunga (Tabora) na Nyengedi (Lindi), na kuimarishwa kwa vituo kama hivyo vya Luhira (Ruvuma) na Kingolwira (Morogoro).

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika sekta ya **viwanda**, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilisha uthamini wa mali za wananchi watakaohama eneo la Mchuchuma na Liganga, kulipa fidia ya shilingi bilioni 7 katika eneo la uwekezaji Bagamoyo kwa ajili ya kujenga bandari na eneo la viwanda. Vile vile, ufungaji wa mitambo na ujenzi wa miundombinu ya kiwanda cha Viuadudu – Kibaha upo katika hatua za mwisho. Aidha, katika eneo la EPZA (Mabibo) lenye sehemu ya viwanda 16, viwanda 13 vimekamilika ambapo viwanda 6 vinafanya kazi na viwili vipo katika majaribio.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **sekta binafsi**, hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kukamilika ujenzi na kuanza uzalishaji katika kiwanda cha kukamua mafuta ya mbegu za pamba na alizeti cha Jaelong (Shinyanga); kiwanda cha saruji cha Dangote (Mtwara); kiwanda cha nguo Dahong (Shinyanga); na kiwanda cha usindikaji wa ngozi - Meru (Arusha).

39. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **maendeleo ya rasilimali watu**, hatua iliyofikiwa ni pamoja na kuendelea kugharamia wanafunzi 159 wanaopata mafunzo katika fani za mafuta na gesi kwa ngazi mbalimbali ndani na nje ya nchi ambapo wanafunzi 124 wanagharamiwa na Serikali na wanafunzi 35 wanagharamiwa na nchi wahisani. Aidha, Serikali ilitoa mikopo kwa wanafunzi 99,590 wakiwemo 2,117 wa stashahada za elimu ya ualimu wa masomo ya sayansi na hisabati na hivyo kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya juu. Vile vile, Serikali ilitoa ruzuku kwa wanafunzi 1,793 wanaosomea shahada za udaktari wa binadamu, meno na mifugo katika vyuo vya elimu ya juu sawa na asilimia 94.3 ya lengo.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **sekta ya fedha**, hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kuongeza mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo shilingi bilioni 60; kuendelea kuongeza mtaji wa Benki ya Rasilimali kufikia shilingi bilioni 212 ambapo mtaji kutoka Serikalini ni shilingi bilioni 152.2 na shilingi bilioni 59.8 zimetokana na malimbikizo ya faida. Vile vile, Benki ya Rasilimali imetoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 413. Benki ya wanawake imeongezewa mtaji hadi kufikia shilingi bilioni 8.75 na kutoa huduma za mikopo ambapo idadi ya wanawake waliopewa mikopo walikuwa 25,557 sawa na asilimia 89 ya wakopaji wote na wanaume 3,159 sawa na asilimia 11.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **huduma za utalii,** kazi zilizofanyika ni pamoja na: usanifu wa ujenzi wa awamu ya pili wa jengo la Kitega Uchumi cha Utalii Dar es Salaam; na kuboreshwa kwa mfumo wa ukusanyaji mapato ya utalii, uwindaji na upigaji picha. Mapato yatokanayo na utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.81 mwaka 2013 hadi dola bilioni 1.98 kwa mwaka 2014.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **biashara,** hatua iliyofikiwa ni: kulipwa kwa fidia ya shilingi bilioni 53 katika eneo la kujenga kituo cha Biashara na Huduma Kurasini; kurekebisha sheria ya mfumo wa stakabadhi ghalani na kutoa elimu kwa wadau kuhusu mfumo huo; kuanzishwa kwa kampuni ya *Tanzania Mechantile Exchange plc* kwa ajili ya kusimamia na kuendesha soko la mazao ya bidhaa; na kuhamasisha matumizi ya fursa za masoko ya mipakani, kikanda na kimataifa. Vile vile, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia Sekta Binafsi kushiriki katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2014/15 yapo katika Kitabu cha Mpango wa Maendeleo, sura ya pili **(Uk 9 hadi 54).**

Changamoto na Hatua Zilizochukuliwa

44. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hatua za utekelezaji zilizofikiwa, baadhi ya changamoto zilizojitokeza ni: ufinyu wa rasilimali fedha kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo; madeni hususan ya ujenzi wa miundombinu kama barabara na viwanja vya ndege; ufuatiliaji, tathmini na taarifa hafifu za utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na ugumu wa kupata taarifa za ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji kwenye maeneo ya Mpango. Hii inatokana na sekta binafsi kutokuwa tayari kuruhusu taarifa zao zijulikane kwa washindani wao kibiashara, na baadhi yao kuficha taarifa ili zisitumike katika ukokotoaji wa kodi.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali itaendelea kuongeza wigo wa kodi na kuimarisha ukusanyaji wa mapato, ikiwa ni pamoja na kusimamia kikamilifu matumizi ya vifaa vya kielektroniki kukusanya kodi na kuendelea kuhamasisha Sekta Binafsi ili waweze kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Usimamizi

na Ufuatiliaji, itaendelea kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya Matokeo Makubwa Sasa. Vile vile, Tume ya Mipango kwa kushirikiana na sekta mbalimbali itaendelea kufuatilia miradi mingine mikubwa ya kimkakati.

MALENGO YA MPANGO NA MIRADI YA KIPAUMBELE 2015/16

46. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuelezea Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16, naomba kusisitiza kuwa Mpango huu umezingatia maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16). Vile vile, Mpango huu umezingatia Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini – MKUKUTA II, Malengo ya Milenia (2015), Agenda ya maendeleo baada ya 2015, Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2015/16, Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2015/16 yaliyojadiliwa na Bunge hili Novemba 2014, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2010 – 2015) na sera na mikakati ya kisekta.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuainisha kwa muhtasari maeneo muhimu ambayo Kamati ya Bunge ya Bajeti ilishauri yazingatiwe katika Mpango. Maeneo hayo ni pamoja na: kudhibiti mfumuko wa bei na kushuka kwa thamani ya shilingi; kuongeza nguvu katika kupunguza umaskini wa kipato na kuongeza fursa za ajira hasa kwa vijana; kuanza ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa cha *Standard gauge*, kuharakisha upatikanaji wa umeme wa uhakika hususan vijijini; kuboresha huduma za maji vijijini; kilimo cha umwagiliaji; mazingira ya uwekezaji kwa Sekta Binafsi; upatikanaji wa huduma bora za elimu na afya; na kuimarisha sekta za mifugo na uvuvi; Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maeneo haya yote yamezingatiwa ipasavyo katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16.

Malengo na Masuala Muhimu Yaliyozingatiwa katika Mpango

48. ***Mheshimiwa Spika,*** malengo yaliyozingatiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16 ni kama ifuatavyo:-

i. Kudumisha amani na umoja nchini sambamba na kuimarisha Utawala bora;
ii. Kupunguza umaskini;
iii. Kuimarisha utengamavu wa viashiria vya uchumi jumla;

iv. Kuongeza thamani ya mazao, mifugo, uvuvi na madini;
v. Kuongeza maghala na kuimarisha masoko ya mazao;
vi. Kuvutia watalii wengi na kukuza utalii wa ndani; na
vii. Kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** masuala muhimu yaliyozingatiwa katika Mpango wa Maendeleo 2015/16 ni:

i. Kukamilisha miradi inayoendelea, hususan ile ya Matokeo Makubwa Sasa;
ii. Kuhakikisha usalama wa chakula nchini;
iii. Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji;
iv. Kupanua fursa za ajira;
v. Kuendeleza rasilimali watu hususan katika nyanja za mafuta na gesi, sayansi, ubunifu, teknolojia na maabara; na
vi. Kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Maeneo ya Kipaumbele, 2015/16

(i) Miradi ya Kimkakati

50. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la miundombinu ya **reli** shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: kupata mwekezaji wa kuanza ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa cha *standard gauge* (mm 1,435); kuboresha miundombinu ya reli ya TAZARA; kukamilisha upembuzi wa kina na kupata mwekezaji wa kuanza ujenzi wa reli mpya ya Mtwara – Mbamba Bay ili kuandaa mazingira mazuri ya utekelezaji wa miradi ya chuma Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma; na kuendelea kuboresha miundombinu ya usafiri wa reli jijini Dar es Salaam.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la **barabara**, Serikali itaendelea kutekeleza miradi inayoendelea, hususan barabara zinazofungua maeneo yenye fursa za kiuchumi na kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa masoko hususan maeneo ya kilimo, ufugaji, madini na utalii.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **bandari,** Serikali itaendelea kuboresha miundombinu na ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kuhudumia shehena, hususan katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Aidha, Serikali itaendea kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa bandari mpya za Mbegani (Bagamoyo) na Mwambani

(Tanga). Vile vile, bandari za Mwanza, Kigoma, Kasanga (Rukwa) na Itungi (Mbeya) zitapewa kipaumbele.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **nishati**, miradi ya umeme vijijini itaendelea kupewa kipaumbele cha juu. Miradi mingine itakayopewa umuhimu wa kipekee ni pamoja na: mitambo ya kufua umeme Kinyerezi I na II; na miradi ya makaa ya mawe ya Kiwira, Mchuchuma na Ngaka. Aidha, kwa upande wa usafirishaji wa umeme, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na: ujenzi na uimarishaji wa njia za umeme wa msongo wa kV 400 North – West Grid; kV 400 Iringa - Shinyanga; kV 400 Dar – Tanga – Arusha; kV 220 Makambako – Songea; na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia ya umeme kutoka Mchuchuma hadi Liganga.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **maji mijini na vijijini**, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa vijiji 10 katika kila Halmashauri, uchimbaji wa visima na mabwawa, na upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji vijijini. Vile vile, Serikali itaendelea kuboresha huduma za maji safi na majitaka katika Jiji la Dar es Salaam kwa kukamilisha miradi ya Ruvu Juu na Chini, mradi wa visima virefu vya Kimbiji na Mpera na ujenzi wa bwawa la Kidunda. Aidha, msukumo utawekwa katika ukarabati wa miundombinu ya miradi ya maji ya Kitaifa ya Chalinze (Pwani), Handeni Trunk Main (Tanga), Masasi – Nachingwea (Mtwara), Mugango - Kiabakari (Mara), Makonde (Mtwara), Maswa (Simiyu) na Wanging'ombe (Njombe). Serikali pia, itaendelea kuongeza upatikanaji wa maji katika miji mingine nchini kwa kuboresha na kuongeza miundombinu na vyanzo vipya vya rasilimali za maji hususan Mtwara – Mikindani, Tabora, Dodoma, Kigoma, Lindi, Sumbawanga, Babati, Kiteto na Arusha.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika sekta ya **kilimo**, miradi itakayopewa kipaumbele ni: kuongeza uzalishaji wa mbegu bora; kuendeleza tafiti za kilimo; na ukarabati wa miundombinu katika vyuo vya mafunzo ya kilimo. Vile vile, Serikali itakamilisha ujenzi wa: miundombinu kwenye skimu 10 za DASIP na skimu 10 kwenye kanda nyingine za umwagiliaji katika mikoa ya Dodoma, Tabora, Mtwara na Kilimanjaro; mabwawa ya maji hususan mabwawa ya Chemba - Kondoa, Gidabahabieg - Hanang, Tarime na Ngorongoro; na kuendelea na ujenzi wa ghala la Makambako na kuanza ujenzi wa ghala la Songea.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **Mifugo**, shughuli zitakazopewa kipaumbele ni: kuboresha miundombinu ya maji na malisho; kuimarisha mashamba ya uzalishaji mitamba; kuimarisha vituo vya uhamilishaji; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa minada; kuongeza upatikanaji wa pembejeo za mifugo; na ujenzi wa vituo vya mafunzo na huduma kwa wafugaji. Aidha, katika eneo la **uvuvi**, shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi; kuimarisha taasisi ya tafiti za uvuvi; kuongeza upatikanaji wa pembejeo za uvuvi; na uzalishaji wa samaki.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la **viwanda** kazi zitakazotekelezwa ni: kuanza kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha miradi ya Mchuchuma na Liganga; kukamilisha usanifu wa mgodi wa chuma pamoja na usanifu wa kujenga kiwanda cha chuma katika eneo la Liganga; kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kuendeleza mradi wa magadi soda Engaruka; na kukamilisha ujenzi wa kituo cha umeme na bwawa la majitaka kwa ajili ya matumizi ya kiwanda cha Viuadudu Kibaha. Aidha, katika eneo la EPZA (Mabibo) kazi kubwa itakuwa ni kuhakikisha viwanda vilivyojengwa vinaanza kazi.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **maendeleo ya rasilimali watu**, kazi zitakazotekelezwa ni: kuendelea na utekelezaji wa miradi ya elimu chini ya utaratibu wa Matokeo Makubwa Sasa; kuendelea kutoa mafunzo katika nyanja maalum hususan mafuta na gesi; kuendelea na ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili Kampasi ya Mloganzila; kuanzisha Chuo Kikuu cha Kilimo, Sayansi na Teknolojia cha Julius Nyerere – Butiama; kuendelea kuboresha miundombinu katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, na kuendeleza elimu ya ufundi stadi. Aidha Serikali itaendelea kutoa mikopo na kuongezeka idadi ya wanafunzi wanaopata mikopo katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

59. ***Mheshimiwa Spika***, katika sekta ya **fedha na biashara:** Serikali itaendelea kuongeza mtaji katika Benki ya Kilimo ili kuanza kutoa mikopo. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha Benki ya Rasilimali na Benki ya Wanawake kwa kuongeza mtaji na kuziwezesha benki hizo kupanua wigo wa huduma; na kuendelea kutekeleza programu ya maboresho katika sekta ya fedha. Vile vile, Serikali itakamilisha malipo ya fidia na kusafisha eneo la ujenzi wa kituo cha Huduma na Biashara Kurasini. Pia, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ili kuvutia Sekta Binafsi

kuongeza kasi ya uwekezaji katika utoaji wa huduma za utalii, biashara na za kibenki.

(ii) Miradi Mingine Muhimu kwa Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini

60. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine muhimu kwa ukuaji wa uchumi itatekelezwa katika sekta za: usafiri wa majini na anga; maendeleo ya jamii; kazi na ajira; misitu na wanyamapori; ardhi, nyumba na makazi; hali ya hewa; madini; utawala bora; vitambulisho vya Taifa; ushirikiano wa kikanda na kimataifa; na mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Ushiriki wa Sekta Binafsi

61. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo 2015/16, Serikali itaelekeza rasilimali fedha zaidi katika miradi mahsusi ya kufungua uwekezaji wa sekta binafsi; kuendelea kutekeleza mapendekezo ya kimaabara ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini; na kuwezesha utekelezaji wa sheria ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Aidha, Serikali itaendelea na programu za kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia urasimishaji wa biashara za wajasiriamali wadogo na maendeleo ya SACCOS na VICOBA. Vile vile, Serikali itaendelea kuweka msisitizo katika kurasimisha rasilimali za wananchi kupitia MKURABITA.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu maeneo ya kipaumbele yapo katika Kitabu cha Mpango wa Maendeleo, sura ya tatu **(Uk 55 hadi 81).**

UGHARAMIAJI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2015/16

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, makadirio ya mahitaji ya fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 5,979.7 ambapo shilingi bilioni 4,317.5 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1,662.2 ni fedha za nje. Kwa ujumla sehemu kubwa ya fedha za ndani za maendeleo zimeelekezwa katika maeneo ya kipaumbele ya miundombinu (barabara, reli, bandari, maji, umwagiliaji na TEHAMA); kilimo ikiwemo mifugo na uvuvi; viwanda;

na elimu na afya. Aidha, Serikali itaendelea kugharamia miradi ya maendeleo kupitia vyanzo vingine vya fedha kama vile, ubia kati ya sekta ya umma na binafsi pamoja na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi kuwekeza katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu ugharamiaji wa utekelezaji wa Mpango yapo katika Kitabu cha Mpango wa Maendeleo, sura ya nne **(Uk 82 hadi 84).**

UFUATILIAJI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Tume ya Mipango itafuatilia na kutathmini miradi ya kitaifa ya kimkakati kwa kushirikiana na sekta. Aidha, Ofisi ya Rais, Utekelezaji na Ufuatiliaji wa Miradi itafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa viashiria vya utekelezaji katika miradi ya Matokeo Makubwa Sasa. Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI itaratibu ufuatiliaji na tathmini ya miradi itakayotekelezwa katika ngazi za Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango yapo katika Kitabu cha Mpango wa Maendeleo, sura ya tano ya **(Uk 85 hadi 91).**

HITIMISHO

67. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kueleza hali ya uchumi wa Taifa, matarajio, mwenendo wa ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2014 na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/15, ni dhahiri kuwa Serikali imepiga hatua kubwa katika kutekeleza program na miradi mbalimbali ya maendeleo. Napenda kwa niaba ya Serikali kuwapongeza wananchi kwa mchango mkubwa uliopelekea kupatikana mafanikio niliyoeleza katika utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo. Napenda vile vile, kuipongeza sekta binafsi na kuiomba iongeze ushiriki wake katika kuanzisha, kuendeleza na kukamilisha miradi iliyopo katika Mpango huu.

68. ***Mheshimiwa spika***, ni ukweli usiopingika kuwa, maendeleo hayawezi kupatikana kwa kutegemea uwekezaji wa Serikali peke yake. Naomba kutoa rai kwa sekta binafsi na kwa Watanzania wote kushiriki kikamilifu katika kuwekeza katika miradi ya maendeleo ya

kipaumbele. Uwekezaji huo utapunguza hatua kwa hatua utegemezi wa kibajeti. Aidha, nawahimiza Watanzania wenzangu kufanya kazi kwa bidii na kwa ufanisi ili kuongeza tija katika uzalishaji. Mipango peke yake haitoshi kuleta matokeo tunayotarajiwa kama hatujipangi kikamilifu na kujituma kwa moyo. Tukumbuke daima kuwa mafanikio yanategemea jitihada za pamoja ambapo Serikali, sekta binafsi na jamii zikishiriki kikamilifu tutapata thamani halisi ya rasilimali zetu katika utekelezaji wa mpango huu wa maendeleo.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine tena napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wake. Katika kipindi chake cha uongozi, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi 20 duniani ambazo uchumi wake unakuwa kwa kasi kubwa (wastani wa zaidi ya asilimia 7) na inakaribia kufikia kundi la nchi zenye uchumi wa kati. Katika kipindi cha miaka 5 iliyopita, kasi ya kupunguza umasikini nchini imeongezeka maradufu ikiwa ni mara ya kwanza katika miaka 15 ya hivi karibuni. Kwa upande mwingine, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi 10 bora katika bara la Afrika kwa kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje kutokana na utulivu wa kisiasa, uchumi wa soko ulioimarika, soko kubwa la watu wapatao milioni 50 na rasilimali asili nyingi. Aidha, Mheshimiwa Rais ametoa mchango mkubwa sana Duniani katika jitihada za kufikia malengo ya milenia ikiwa ni pamoja na kupunguza vifo vya kina mama na watoto. Maendeleo ya nchi yeyote yanatokana na mipango madhubuti. Bila shaka tunakubaliana kwamba kupanga ni kuchagua. Tunachagua kutokana na rasilimali chache tulizonazo ili kutekeleza mpango wetu wa Taifa.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kumaliza hotuba yangu napenda kumshukuru Waziri wa Fedha Mheshimiwa Saada Mkuya Salum (Mb) kwa ushirikiano aliotupatia wakati wote wa maandalizi ya kutayarisha taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo. Aidha, nawashukuru Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Gavana wa Benki Kuu, Mtendaji Mkuu wa PDB, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Kamishina Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ushirikiano waliotupatia. Vile vile, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango wakiongozwa na Katibu Mtendaji Dkt. Philip I. Mpango na watendaji wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Servacius B.

Likwelile kwa kusimamia vizuri kazi za kila siku na maandalizi ya taarifa ya hali ya uchumi, Mpango na hotuba hii.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na vitabu vya Hali ya Uchumi 2014 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16 vinapatikana katika tovuti ya Tume ya Mipango www.mipango.go.tz.

72. ***Mheshimiwa Spika***, naomba sasa Bunge lako Tukufu, lijadili na kupitisha taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa 2014 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.